# JARIDA LA MWEZI

TOLEO NA. 058 AGOSTI 2025

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY




## 1 TMA YATUMIA FURSA YA MAONESHO YA NANENANE KUTOA ELIMU KWA JAMII

## 2 DKT. LADISLAUS CHANG'A ASHIRIKI KATIKA MKUTANO WA 6 WA MAWAZIRI NA MAMLAKA ZA MAZINGIRA WA ASIA NA PASIFIKI




## 3 FAHAMU ZAIDI: HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2025



KITAIFA

# TMA YATUMIA FURSA YA MAONESHO YA NANENANE KUTOA ELIMU KWA JAMII

**Dodoma, Morogoro, Zanzibar, Mbeya**




Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilitumia fursa ya maonesho ya NaneNane 2025 kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Nzuguni, Dodoma, Viwanja vya NaneNane, Morogoro, Viwanja vya Kizimbani - Dole, Zanzibar na Viwanja vya NaneNane, Mbeya kutoa elimu kwa jamii kuhusu huduma zitolewazo pamoja na jukumu kubwa la TMA la kudhibiti shughuli za hali ya hewa nchini.

Kupitia maonesho hayo, wananchi na wadau mbalimbali wakiwemo wakulima, wavuvi na wafugaji walipata elimu ya moja kwa moja kutoka kwa wataalamu wa TMA wakiwemo viongozi.

TMA ilieleza namna taarifa za hali ya hewa zinavyokusanywa, kuchakatwa na kuchambuliwa kupitia mifumo ya kisasa, na jinsi huduma hizo zinavyoweza kusaidia jamii. Aidha, TMA ilieleza umuhimu wa kuendesha shughuli za hali ya hewa zenye kukidhi viwango vya kitaifa na kimataifa.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt.




Ladislaus Chang'a na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Kimataifa la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), akiwahudumia wateja kwenye banda la Mamlaka aliwahimiza wadau wote kufuatilia utabiri wa kila siku, utabiri wa msimu pamoja na tahadhari za hali mbaya ya hewa, huku akisisitiza matumizi sahihi ya taarifa hizo katika shughuli zote za kiuchumi na kijamii.

Aidha, aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya hali ya hewa na rasilimali watu na hivyo kuleta maendeleo makubwa ya utendaji kazi wa Mamlaka.

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ilishiriki katika maonesho ya NaneNane Dodoma, Zanzibar, Mbeya na Morogoro na kupata zawadi ya kombe la mshindi wa nafasi ya pili. Ushindani uliyohusisha taasis za Serikali upande wa Mawakala na Mamlaka za Serikali nchini. Kauli Mbiu ya mwaka huu ni "Chagua Viongozi Bora kwa Maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi 2025".



## KIMATAIFA

# DKT. LADISLAUS CHANG'A ASHIRIKI KATIKA MKUTANO WA 6 WA MAWAZIRI NA MAMLAKA ZA MAZINGIRA WA ASIA NA PASIFIKI

**Nadi, Fiji**



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Makamu Mwenyekiti wa Jopo la Sayansi ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na Tabianchi (IPCC), Dkt. Ladislaus Chang'a, kwa mwaliko wa Programu ya Umoja wa Mataifa uratibu wa Mazingira (UNEP) alishiriki kikamilifu katika Mkutano wa 6 wa Mawaziri na Mamlaka za Mazingira wa Asia na Pasifiki (6th AP Forum) uliofanyika kuanzia tarehe 26–29 Agosti 2025 Jijini Nadi, Fiji. Mkutano huo uliandaliwa kwa pamoja na Serikali ya Fiji na UNEP ukiwa na kaulimbiu "Kutafuta Suluhisho Endelevu katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi Duniani".

Sambamba na mkutano huo, Dkt. Chang'a alikuwa na vikao mbalimbali na waheshimiwa na taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kikao na Mhe. Rupa B. K., Waziri wa Serikali ya Nepal, Wizara ya Misitu na Mazingira, ambapo alimpatia taarifa kuhusu mpango kazi wa IPCC unaotekelezwa hadi mwaka 2029. Mazungumzo hayo yalijikita katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuboresha sera za

mazingira. Mhe. Rupa alishukuru na kupongeza sana kazi kubwa inayofanywa na IPCC.

Aidha, Dkt. Chang'a alishiriki na kuratibu kikao cha ngazi ya Mawaziri kuhusu Mfumo wa Tahadhari za Majanga ikiwa ni pamoja na yale yanayosababishwa na hali ya hewa. Kikao hiki cha Waheshimiwa Mawaziri wa Asia na Pasifiki kilikuwa na wazungumzaji (panelists) wakiwemo: Mhe. Thoriq Ibrahim, Waziri wa Utalii na Mazingira wa Maldives; Mhe. Bi. Mona Ainu'u, Waziri wa Rasilimali Asili wa Niue; Mhe. Dkt. Maina Vakafua Talia, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira wa Tuvalu; Bi. Fleur Downard, Mkurugenzi wa Masuala ya Mazingira ya Kimataifa na Kitengo cha Umoja wa Mataifa, Wizara ya Mabadiliko ya Tabianchi, Nishati, Mazingira na Maji, wa Australia; na Bw. Sefanaia Nawadra, Mkurugenzi Mkuu, Sekretarieti ya Programu ya Mazingira kanda ya Pasifiki (Pacific Regional Environment Programme-SPREP).

Kikao hicho kiliangazia umuhimu wa mifumo ya tahadhari za majanga (multi-hazard early warning systems-MHEWS) kama mojawapo ya hatua bora zinazotekelezeka katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi, kwa lengo la kulinda maisha na mazingira".

Mkutano huu wa 6 wa Waheshimiwa Mawaziri wa Asia na Pasifiki wenye dhamana ya sekta ya mazingira ulikuwa pia jukwaa muhimu kwa makundi mbalimbali katika ukanda huo kuwakilisha serikali zao, mashirika ya kikanda, vijana, sekta binafsi na wadau ambapo mchango na maoni yao vitasaidia katika maandalizi ya Mkutano wa 7 wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira (Seventh Session of the United Nations Environment Assembly (UNEA-7) unaotarajiwa kufanyika mwezi Desemba 2025 jijini Nairobi, Kenya.



TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

## FAHAMU ZAIDI

### HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA, 2025

Kipindi cha mwezi Septemba 2025, maeneo mengi ya nchi yanatarajiwa kuwa na hali ya baridi kiasi, na viwango vya chini zaidi vya joto vinatarajiwa kuendelea katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi. Aidha, ongozeko kidogo la joto linatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Vipindi vifupi vya upepo mkali vinatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo, hususan ya ukanda wa pwani na maziwa makuu. Kwa upande wa mvua, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache, hususan yale yalioko ukanda wa pwani, Ziwa Victoria na maeneo ya miinuko ya nyanda za juu kaskazini mashariki.

| MAENEO | MAELEZO |
|---|---|
| Pwani ya Kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 18 °C hadi 25 °C katika maeneo ya mwambao wa pwani na visiwani. Kwa maeneo ya nchi kavu kati ya nyuzi joto 14 °C na 20 °C. Kiujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi. **Aidha, vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Nyanda za juu Kaskazini Mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, baadhi ya maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na viwango vya chini ya nyuzi joto 12 °C. **Kwa ujumla, hali ya ukavu inatarajiwa katika maeneo mengi, huku vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa hususan katika maeneo ya miinuko.** |
| Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 22 °C katika maeneo mengi. Hata hivyo, maeneo ya miinuko ya mikoa ya Kagera na Geita yanatarajiwa kuwa na kiwango cha chini ya nyuzi joto 14 °C. **Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.** |
| Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 14 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. **Kwa upande mwingine, hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 12 °C hadi 20 °C katika maeneo mengi. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Nyanda za juu Kusini Magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 8 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Aidha, hali ya baridi zaidi ya kiwango cha chini ya nyuzi joto 8 °C inatarajiwa katika maeneo ya miinuko, ikijumuisha mkoa wa Njombe. **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |
| Pwani ya Kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 15 °C hadi 24 °C katika maeneo mengi. **Aidha, hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa katika maeneo mengi pamoja na vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa kujitokeza katika maeneo machache ya mwambao wa pwani.** |
| Kanda ya Kusini (Mkoa wa Ruvuma): | ♦ Viwango vya joto la chini vinatarajiwa kuwa kati ya nyuzi joto 10 °C hadi 18 °C katika maeneo mengi. Maeneo ya miinuko yanatarajiwa kuwa na kiwango chini ya nyuzi joto 10 °C . **Hali ya ukavu inatarajiwa kuendelea katika maeneo mengi.** |

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Timu ya wataalamu kutoka Kituo cha Kikanda cha Huduma za Hali ya Hewa cha Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika "SADC Climate Service Centre-(SADC CSC) (kulia), walipotembelea ofisi za TMA zilizopo Ubungo Plaza, Dar es Salaam, kwa lengo la kukagua utendaji kazi wa vifaa ambavyo vimetolewa msaada na kituo hicho cha "SADC CSC" kwa Tanzania kupitia TMA.*



*Baadhi ya wanafunzi wa Shule ya Sekondari Ngunya iliyopo Ituha - Mbeya, wakipata mafunzo ya hali ya hewa kutoka kwa mtaalamu wa hali ya hewa, wakati wa Maonesho ya NaneNane 2025, yaliyofanyika katika Viwanja vya NaneNane, Mbeya.*




*Baadhi ya wadau wakipata mafunzo ya huduma za hali ya hewa kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Hali ya Hewa Zanzibar wakati wa maonesho ya NaneNane yaliyofanyika katika viwanja vya Kizimbani - Dole, Zanzibar.*




*Baadhi ya wataalam wa hali ya hewa wakiwa wamebeba zawadi ya kombe la mshindi wa nafasi ya pili, baada ya Maonesho ya NaneNane 2025, yaliyofanyika katika Viwanja vya NaneNane Morogoro. Ushindani ulihusisha taasisi za Serikali upande wa Mawakala na Mamlaka za Serikali nchini.*





**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

**Mhariri**
Monica Mutoni

**Waandishi**
Monica Mutoni
Wilbert Muruke

**Msanifu Kurasa**
Kennedy Mgeta

**Shukrani**
Kituo Kikuu cha Utabiri
Ofisi ya Ushirikiano wa Hali ya Hewa Kimataifa



www.meteo.go.tz

@tma_servces

@tanzaniameteorological

www.meteotz1950.blogspot.com

TMAonline_TV

WhatsApp channel
**Tanzania Met Authority**

Scan hapa kujiunga

Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu,
1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27,
41218 DODOMA.